



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKINOLOJIA YA ABARI  
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED



**TAARIFA KWA UMMA**

**USAFIRISHAJI VIFURUSHI NA VIPETO BILA KUWA NA LESENI**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya 2003, na kupewa jukumu la kusimamia Sekta ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta nchini Tanzania.

Katika kutekeleza majukumu yake, TCRA imebaini kuwepo kwa Kampuni (Mabasi) au watu binafsi wanaofanya biashara ya usafirishaji vifurushi na vipeto bila kuwa na Leseni kutoka TCRA.

Kwa mujibu wa Kifungu, cha 36 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Namba 3 ya 2010, mtu yeyote haruhusiwi kutoa huduma za Posta/Vipeto katika Jamhuri ya Muungano isipokuwa kama mtu huyo ana leseni iliyotolewa na TCRA.

TCRA, inautaarifu umma na wafanyabiashara ya mabasi wote wanaotoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto bila kuwa na leseni kutoka TCRA kuhlalisha huduma hiyo kwa kupata leseni kutoka TCRA kabla ya tarehe 31 Oktoba,2021.

Kwa ambaye atashindwa kutekeleza ilani hii, TCRA itakuchukua hatua stahiki za kisheria bila kutoa taarifa nyingine.

**IMETOLEWA NA  
MKURUGENZI MKUU  
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA  
9 Septemba, 2021**